

Mchango wa Mohammad bin Abu Bakari Omar al-Bakry Kijumwa katika Utamaduni wa Amu

Tom Olali

Ikisiri

Makala haya yanadhamiria kuchunguza mchango wa Mohammad bin Abu Bakari Omar al-Bakry (maarufu kama Kijumwa) katika maendeleo ya utamaduni wa Waswahili wa kisiwa cha Amu (Lamu), Kenya. Makala haya yanamrejelea Mohammad bin Abu Bakari Omar al-Bakry kama Kijumwa na kisiwa cha Lamu kama Amu. Makala yanapiga darubini mchango wake katika fani mbili: fani ya utamaduni, hususan sanaa ya useremala na vilevile fani ya fasihi ya Kiswahili. Tunatoa hoja kuwa utamaduni wa Waswahili wa Amu umekuzwa na talanta ya Kijumwa na kwamba mchango wake umechangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya utamaduni wa Waswahili wa Amu. Pili, tunatoa hoja kuwa mchango wake katika uwanja wa fasihi si haba na umechangia katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili ijapo lengo la makala haya hasa ni kuona jinsi mchango wake ulivyokuza sanaa ya fasihi katika kisiwa cha Amu. Sehemu ya data katika kuandika makala haya ilikusanywa katika miaka ya 2000 na baadhi ya habari zilizotolewa humu hazijachapishwa bali zimenaswa kwenye tepu za kunasa sauti na kumilikiwa na mwandishi.

1.0 Historia ya Kijumwa

Kijumwa alizaliwa mnamo mwaka 1855 (Olali, 2004; 2008a). Kwa mujibu wa jamaa zake, Kijumwa aliishi kwa muda wa miaka 90 na kufariki muda mfupi kabla ya Vita Kuu vya Pili vya Dunia mwaka 1945. Wazazi wote wa Kijumwa walizaliwa Amu. Habari kuhusu maisha yake ya utotoni haikuhifadhiwa na mengi sana kuhusu maisha yake hayajulikani. Kama walivyo watoto wengi wadogo wa kisiwani Amu, Kijumwa alipitia elimu ya madrasa. Akiwa katika madrasa, alionyesha talanta kubwa hasa katika musabaka (kule kuhifadhi na kukariri aya za Korani) na pia sanaa ya kuandika herufi za Swarabi.

Kijumwa aliendeleza talanta yake na kuwa shaha (bingwa wa kutunga mashairi). Pia, alionyesha talanta katika sanaa ya useremala, utungaji wa tendi, mashairi, ukuzaji wa miswada, utribu, utafsiri, historia simulizi, ufumaji wa kofia, ushonaji, muziki, utungaji wa nyimbo, utengenezaji wa ala za muziki (hasa kibangala) na hatimaye akawa msanii mahiri na hivyo akapewa jina Kijumwa (yule aliyebobea katika sanaa). Kijumwa alilelewa akiwa ni mwanafalsafa hodari kutokana na tabia yake ya kuuliza maswali mengi kuhusu mambo mbalimbali ya maisha. Mchango wake katika uwanja wa sanaa ya fasihi andishi na simulizi ni wa kipekee. Mathalani, ushairi ulimtosha katika masuala ya kitamaduni kama vile

mashindano ya kucheza dansi na beni. Wakati wa beni za miaka ya 1920, Kijumwa alikuwemo kwenye kundi la Kambaa ambapo alitunga nyimbo nyingi na mashairi kulitukuza kundi lake na yale yaliyokuwa yanawakejeli kundi pinzani la Skochi (Scott) lililoongozwa na Bwana Zena (Olali, 2012). Mfano mzuri ni huu:

*Rabi takupa kigongo,
Na kisu cha kukuwasha,
Mungu akupe ushingo,
Upite ukikupisha,
Mungu takupa Zifungo,
Usifunguke maisha.*

2.0 Talanta za Kijumwa

Kama tulivyoeleza hapo awali, Kijumwa alikuwa mahiri katika fani kadhaa, ufafanuzi wa vipaji vyake tunautoa hapa chini:

2.1 Mchongaji Bingwa

Katika talanta zake zote alizokuwa nazo Kijumwa, uchongaji ulikuwa unashikilia nafasi kubwa sana maishani mwake. Kijumwa alilelewa katika mazingira ya uchongaji wa samani, hususan milango na samani nyingine ambazo mwanzoni zilitoka Siu kabla ya mwaka 1800. Kutekwa kwa upwa wa Afrika Mashariki na Waarabu wa Omani na baadaye kuhamishwa kwa jiji kuu kutoka Muscat hadi Zanzibar na Sultani Sayyid Said mnamo mwaka 1840, kulisababisha kuingizwa kwa aina nyingi ya milango na samani hasa kutoka India, Uajemi na Uchina. Huu ndio wakati ambapo milango mbalimbali iliingizwa kama vile milango yenye nakshi za Kiomani, Gujerati na Unguja. Kabla ya milango yenye nakshi za Kiomani kuingizwa pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1750, milango mingi yenye nakshi na pia samani ambayo ilikuwa iko Lamu ilitoka Siu ama Pate. Wakati huu kulikuwa na watu wachache wenye vipawa katika masuala ya samani ambao waliweza kutia nakshi ndogondogo, maridadi na yenye kuvutia inayopatikana katika milango ya Omani. Mlango wa zamani kabisa ulio na nakshi za nje unapatikana katika msikiti wa N'nalalo nao ni wa mwaka wa 1796 (Olali, 2008a).

Mjini Amu, mlango katika duka kubwa la jumla la Salim Ali Swaleh ulichongwa awali kabisa ukilinganishwa na mlango wa makavazi ya Lamu na mlango wa makavazi ya Posta ya Wajerumani. Hata hivyo, katika mlango wa makavazi ya Posta ya Wajerumani ambao uliidhinishwa na jamii ya Denhardt mnamo mwaka 1893, Kijumwa aliweza kuonesha ubingwa wake katika kutia nakshi, uchongaji na pia maandishi. Mradi wake mkuu ni mlango wa makavazi ya Lamu. Hata hivyo, mlango unaovutia wengi kabisa ni ule wa Jumba la Liwali ambalo yumkini limechota mengi kutoka milango mikuu ya Unguja yenye linta nusu duara na taji la kifalme juu. Milango yake inaonesha kuwa safari zake za

Unguja kucheza taarabu pia ilimwezesha kupata nafasi ya kuimarisha talanta yake katika utiaji nakshi na uchongaji wa samani.

Pia, milango ambayo yumkini ilichongwa na Kijumwa, kwa sababu ina mtindo mmoja wa nakshi, ni ile ya Kenya Commercial Bank na milango ile miwili inayopatikana katika nyuma ya jengo la Makavazi ya Lamu. Ukiangalia kwa makini kabisa utaona kwamba nakshi za Kijumwa, hususan zile zinazoonekana kama maua ni athari ya nakshi za Omani. Hii pia inathibitika katika Kofia ya Waswahili wa Amu. Kijumwa alianza mafunzo yake ya uchongaji kutoka kwa fundi Hamadi na Fundi Shee Jumaa. Akitumia ufundi wa kimsingi kabisa katika uchongaji aliojifunza kutoka kwa walimu wake, Kijumwa alipiga hatua moja mbele na kuifinyanga mitindo mipya ambayo iliathiriwa na mazingira yake na matakwa ya mteja wake.

Kijumwa alikuwa ni fundi wa mafundi kwa takriban kila kitu alichotaka au pengine hata kutakiwa kufanya. Kwa mfano, wakati Sultani Omari bin Mohammed wa Witu alipofariki mnamo mwaka 1923, rafiki zake Sultan wenye asili ya Kijerumani walimwambia alifinyange Jiwe la Kaburi (Olali, 2012). Wakati Liwali Seif bin Salim alipoujenga msikiti karibu na kituo cha Kengen kilichoko usita wa mui (mbele ya mji), alimwagiza Kijumwa kubuni na kufinyanga kibla. Wakati huo, jahazi la mtepe ambalo lilifumwa bila matumizi yoyote ya misumari lilitoweka na badala yake kuingizwa kwa jahazi jipya na la kisasa. Kipindi hicho kulitokea haja ya kutia nakshi kwenye omo (au gubeti). Ile rangi ya awali nyeusi na nyekundu ambayo ilikuwa ikitumika kwenye mtepe haikupokelewa vizuri kwenye jahazi jipya. Kijumwa aliona umuhimu wa kutia nakshi tofauti katika omo ama gubeti ya jahazi jipya na hivyo akaja na nakshi ya maua mapya kabisa yaitwayo mapi ambayo mpaka hivi sasa yanatumika kama nakshi katika majahazi ya Amu.

2.2 Mtengenezaji Kibangala

Kama mwanamuziki, Kijumwa alihakikisha kwamba alijenga na kufumua ala zake za muziki. Ingawa aliunda aina mbalimbali za ala za muziki, ile ambayo ilikuwa maarufu kuzidi zote ni kibangala ambacho baadaye kilijulikana kama 'ala yake'. Kwa hakika haijulikani ni nani aliyemfunza kukiunda kibangala hicho, kwa sababu ala kama hii pia ilipatikana Indonesia na Komoro 2008b). Hata hivyo, kibangala cha Kijumwa kilikuwa tofauti katika umbo lake. Kibangala cha Kijumwa kilijengwa kutoka kipande kimoja cha mti, kazi ambayo haikuwa rahisi kuitimiza katika uchongaji.

2.3 Mwalimu wa Sanaa

Kijumwa alikuwa na mtoto mmoja tu wa kiume kwa jina Helewa ambaye naye alimfunza sanaa ya uchongaji. Tofauti na babake, Helewa alikuwa mtu mpole na hakuwa mbishani kama alivyokuwa babake. Helewa alilelewa Amu lakini

alipokuwa na umri wa miaka 15 alitoka Lamu kwenda Unguja ambapo aliajiriwa kama seremala. Mnamo mwaka 1945, alirudi Amu lakini maisha yalikuwa magumu sana na mnamo mwaka wa 1949, aliamua kwenda Mombasa.

Mwingine ambaye alipata mafunzo kutoka kwa Kijumwa alikuwa ni Skanda. Mojawapo ya milango ya Skanda ni wa jumba la Fakrudin uliochongwa mnamo mwaka 1971. Huu ni mlango mmojawapo wa milango ya kuvutia mjini Amu. Skanda alipata zile nakshi kutoka mlango wa makavazi ya Posta ya Ujerumani. Aliongeza nakshi chache kwenye taji na kupata lintu nusu. Skanda pia kwa mara ya kwanza alitumia nakshi za Kijumwa za mlangoni kwenye makasha na samani nyingine. Kwa mujibu wa utafiti wetu, Skanda amejihusisha na miradi mingi kote ulimwenguni 2011. Miongoni mwa kazi zake ni mlango wa futi 30 wa Mama Ngina Kenyatta. Wanafunzi maarufu wa Skanda ni pamoja na Abdalla Swaleh, Ahmed Kureish, Bakar Sheika, Athman Skanda, Athman Hussein, Mohammed Zein mbali na wengine.

Kwa upande wa fasihi Kijumwa enzi za uhai wake alifanya mambo kadha wa kadha kama ifuatavyo:

2.4 Mkuza Miswada ya Kifasihi

Werner (1934) anaona kuwa hakuna mtunzi wala mkuza miswada aliyechangia, kufanikisha na kunawirisha fasihi ya Kiswahili kuliko Kijumwa wakati wa enzi zake. Kulingana na Abou E. Ibrahim (1983), mhakiki wa maisha na kazi ya Kijumwa, anaelezea kuwa Kijumwa alifanikiwa kutunga, kuandika, kutafsiri, kuhariri na kukusanya kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili, kazi hizo zimejikita kwenye makundi makuu manne nayo ni:

- a) Kazi alizozitunga mwenyewe na kuwanakilia wataalamu wa kigeni kwa hati za Kirumi;
- b) Kazi alizozitunga mwenyewe lakini akatia majina ya watunzi wengine au akawaeleza wataalamu wa Kizungu kwamba watunzi hawajulikani, kwa sababu ya hali yao kiuchumi, kisiasa na kidini;
- c) Kazi alizozitafsiri kutoka Kiarabu na baadaye kuzinukuu; na.
- d) Kazi alizozitafsiri kutoka lahaja ya Kimvita hadi ya Kiamu.

Ufafanuzi wa baadhi ya kazi hizo tunautoa hapa chini:

a) **Kazi Alizozitunga na Kuwanakilia Wataalamu wa Kigeni kwa Hati ya Kirumi**

Knappert (1967) anaelezea kuwa Kijumwa alitunga tungo zake kuhusu takriban kila kitu. Alibuni tungo kutoka hadithi za *Biblia Takatifu* na pia kutoka *Qu'ran Takatifu*. Mawazo haya ninayaunga mkono kwani tungo ninazozirejelea ni zenye ubunifu na za kutamaniwa na wengi kwa weledi wa kufinyanga lugha na kuibua fasihi yenye mafunzo ya falsafa ya jamii. Majowapo ya kazi zake ni *Utendi wa Njiwa na Kozi*, huu ni utungo maarufu ambao una mafunzo yanayoelekeza

kutoshawishiwa na matendo yasiyotufaa. Utendi wenyewe ni wa kimajibizano baina ya Nabii Musa, malaika Mikaili na Jibrili ambao wamejifanya Kozi na Njiwa (aina za nyuni). Utendi huu una beti 37. Hata hivyo, utendi maarufu sana wa Kijumwa ni *Utendi wa Fumo Liyongo* ambao alikutunga mwaka 1913. Utendi huu ni maarufu na unasimulia sira ya ujinga wa Fumo Liyongo. Utendi huu una maudhui ya migongano ya wenyeji na utawala wa Kisultani, na pia husawiri mifumo ya kijamii. Utendi huu umehaririwa na wahakiki wengi akiwemo Hichens, Allen na Werner. Pia, Mulokozi (1999) katika *Tenzi Tatu za Kale* ametoa mchango mkubwa kuhusu sira ya Kijumwa. Kazi hii inatoa habari kuhusu alikozaliwa Kijumwa na nafasi yake miongoni mwa Waswahili wa Amu katika uwanja wa utunzi wa tendi mbalimbali.

Utendi wa *Kisa cha Haramia na KadhiKadhi na Haramiya* wenye beti 234 ni utendi uliotungwa, mwaka 1914 BK na kunakiliwa na Yahya Ali Omar. Utendi huu ni maarufu kwa misingi yake ya kutathmini nguvu za ushawishi wa shetani na hatimaye kuangazia nguvu na uwezo wa Mungu. Dammann (1957) anauchanganua utendi huu na kutueleza jinsi kadhi alivyokabiliana na mwizi kwa kutaka kumnyanga'nya vazi lake, huku kila mmoja akikariri aya kutoka *Qu'ran Takatifu*. *Kisa cha Yusufu* ni utendi uliotungwa mwaka 1913. Asili ya hadithi yenyewe ina misingi ya vitabu vitakatifu vya *Qu'ran Tukufu* na *Biblia Takatifu*. Katika Biblia hadithi inapatikana kwenye Agano la Kale.

Utendi wa Miiraji wenye beti 664 na ambao ni utendi maarufu kwa wafuasi wa dini ya Kiislamu na ambao unahusu safari ya Mtume Muhammadi S.A.W kutoka Bait-al-masjid (Mecca) hadi Bait-al-mukaddas (Yerusalemu) na hatimaye mbinguni, (Olali, 2012) pia unahusishwa naye. Halikadhalika, *Utendi wa Mkunumbi* ni utendi uliotungwa mwaka 1913 na ni moja ya tendi ambazo aliwatungia watunzi, na kuwatafsiria wageni. Ingawa Kijumwa alikuwa stadi katika utunzi wa utendi, hakutaka kuhusishwa na utunzi ambao uliegemea siasa. Alifahamu kuwa siasa ni mchezo mbaya na kwa sababu hiyo, baadhi ya tungo zake hakutaka kuhusishwa nazo. Kwa hivyo, baadhi ya kazi hizi alizozitunga yeye, hakuandika jina lake kama ndiye mtunzi na badala yake, alidai tu kuwa wenye kuzitunga kazi hizo hawakujulikana. Hii ilikuwa ni hatua ya usalama wake kwani yeye hakutaka kujihusisha na siasa abadani!

b) Kazi Alizozitafsiri na Kunakili kutoka Hati ya Kiarabu hadi Hati ya Kirumi

Kijumwa alinukuu na kutarjumi kazi mbalimbali kutoka hati ya Kiarabu hadi Kirumi. Nia yake ilikuwa ni kushughulikia tendi nyingi za kikale. Tendi nyingi zilikuwa maarufu sana baada ya kutafsiriwa kimaudhui na hivyo kuwapa msukumo na motisha wa kutafsiri kazi nyingine. *Al- Inkishafi* ni utendi maarufu sana uliotungwa na Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir (1720-1820) ambao una beti 79. Utendi huu umetolewa miswada mitano na wahakiki wafuatao: Hichens

(1972), J. Allen (1977), R. Allen (1946: 243-249), Harris (1962: 86-102) na Wamlamali (1980, 2011).

c) Kazi Alizozitafsiri kutoka Kiarabu na baadaye Kuzinukuu

Miongoni mwa tendi alizozitafsiri kutoka hati ya Kiarabu hadi kwenye lahaja nyingine ni pamoja na *Siri li Asirari, Wajiwaji, Kasida ya Burdai, Utendi wa Fatuma, Takhmisa ya Liyongo, Herekali, Utendi wa Ayubu* na *Utendi wa Katirifu* (Olali 2004). Halikadhalika, aliunakili *Utenzi wa Mviana Kupona* kutoka hati za Kiarabu hadi kwenye lugha nyingine. *Utendi wa Ngamia na Paa* na *Utendi wa Mkunumbi* vilevile ni miongoni mwa tendi alizoweza kunukuu Kijumwa.

2.5 Mtunzi wa Nyimbo

Kwa mujibu wa Knappert (1967), Kijumwa ametunga nyimbo za nikahi na za tumbuizo. Nyingi ya hizo zilitungwa kati ya mwaka 1700-1800 B.K. Nyimbo zake zilitangulizwa kwa kuporomosha midundo ya ala za muziki kama vile ngoma na pembe. Kama tulivyokwishasema hapo awali, Kijumwa aliongoza kikundi kimoja maarufu cha dansi ya kiutamaduni kilichoitwa Beni. Kikundi chake cha ngoma za kienyeji ndicho kilichoshinda mara kwa mara kwenye mashindano na hafla za nyimbo na dansi za kiutamaduni miongoni mwa jamii ya Waswahili. Aliwahi kutunga wimbo wenye mada muhimu ya wazazi kuwapeleka watoto shuleni. Yumkini nyimbo ambazo alizitunga kuhusu umuhimu wa elimu zilikuwa kichocheo kwa wale viongozi wa Kiislamu, Maliwali na Maimamu ambao waliwakataza jamii ya Waswahili kuwapeleka watoto wao kwenye shule za mfumo wa Ulaya na kupendekeza wasomee madrasa kwani mfumo huo ulilingana na mafunzo ya dini yao. Walihofia watoto wao kukengeushwa na mila na desturi za wakoloni.

2.6 Mtunzi wa Hadithi

Kijumwa pia ni mahiri katika utunzi wa hadithi. Mifano ya hadithi alizotunga ni *Hadithi za Watoto Wanne (Betizo)*. Pia, hadithi ya *Miiraji* ambayo imeandikwa kwa mkono na haijulikani ilitungwa lini. Dammann (1940) anaongeza kuwa *Miiraji* ni kisa ambacho kimefanyiwa uhakiki na wasomi wengi na hata watunzi wengine wa kasida kama vile kasida ya *Umm-al-Qura (Hamziyyah)* na kasida ya *Burudai* wamehusisha kisa hiki cha *Miiraji*. Hadithi nyingine ni zile alizonukuu kutoka lugha ya Kiarabu na kuziandika kwenye lugha nyingine kama vile Kireno na kwa lahaja za Kiswahili. Hadithi hizo miongoni mwa nyingine ni *Hadha Kissat al-Kadhi Ma'ah al-Haramii* (2012).

2.7 Mwandishi wa Wasifu na Barua

Abou (1983) anaelezea kuwa Kijumwa amewahi kuandika wasifu wa Sheikh Mohamed Makata na Sultan Ahmadi. Mswada huu alipewa Werner na baadaye kumkabidhi Hichens huku ukiwa kwenye hati za Kirumi. Mswada wenyewe

ulikuwa kwa hati ya Kiarabu, lakini mtunzi aliweza kuunakili kwa hati za Kirumi. Aidha, Kijumwa aliwaandikia watafiti wa fasihi ya Kiswahili barua kuhusu kusanyo zake kwa hati za Kirumi. Miongoni mwa watafiti wa kizungu aliowaandikia ni Hichens, Taylor, na Dammann. Barua nyingi zilihusu masuala ya utafiti wa fasihi, historia ya Kiswahili na mikusanyiko ya mashairi ya Kiswahili hasa ya eneo la pwani ya Mashariki.

Nyaraka nyingi zilikuwa kati yake na Hichens. Hichens ni mmoja wa wale walionufaika sana kwa kukusanya na kutunukiwa miswada mingi ya fasihi ya Uswahilini. Kulikuwa na barua chache alizoandikiwa na Bwana Whitton, wakala wa forodha ambazo zilihusu kusafirishwa kwa miswada na kupokea chochote alichotumiwa kutoka Uingereza pahali miswada ilipotumwa. Kuna barua tatu kati ya Hichens na Kijumwa akimshukuru kwa miswada na maelezo ya *Utendi wa Hamziyya*, *Utendi wa Ayubu*, *Utendi wa Liyongo*, *Al- Inkishafi* na *Hadithi ya Barasisi* kwani maelezo ya miswada hiyo iliwafaa na kurahisisha kuelewa maudhui na lugha iliyobuniwa kwenye tungo hizo.

2.8 Mfasiri

Kijumwa pia alikuwa mfasiri. Mathalani, alimtafsiria William Taylor kitabu cha Biblia kitiwacho, *The Gospel of St. John* (uk. 72) kutoka lahaja ya Kimvita hadi ya Kiamu. Huenda kulikuwa na tafsiri nyingi alizozifanya kutoka lahaja moja hadi nyingine walakini hazikuwekwa katika kumbukumbu za wahakiki au labda hazikuwa za manufaa kwao.

3.0 Hitimisho

Makala haya yalijikita kuchunguza mchango wa Kijumwa katika jamii ya Amu. Kwa sababu, kwa maoni yetu, mchango wa Kijumwa katika maendeleo ya Kiswahili na utamaduni wa Waswahili ni eneo ambalo halijatafitiwa. Utafiti wetu umedhihirisha kuwa Kijumwa alichangia kwa kiasi kikubwa katika uga wa kisanaa kwa jamii na wanazuoni wa ndani na nje ya Afrika Mashariki. Wapo watu wengi ambao wamechangia mno katika uendelezaji wa Kiswahili na utamaduni wa Waswahili lakini hawajafanyiwa utafiti wa kutosha kung'amua michango yao. Mbali na Kijumwa, huko visiwani Amu, wapo mashaha ambao sifa zao hazijatambulika. Hivyo, tafiti zijazo hazina budi kujikita kutafiti mambo haya.

Marejeo

- Abou, Mohamed. (1983). *Life and Works of Mohammed Kijumwa*, Unpublished PhD. thesis, London: SOAS
- Dammann, E. (1993). *Afrikanische handhireften* (vol.1). Stuttgart.
- Knappert, J. A (1967) *Traditional Swahili Poetry. An Investigation Into the Concepts of East African Islam as Reflected in an Utenzi Literature*: Leiden: E.J. Brill.
- Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Olali, Tom. (2008a). *An English Rendition of a Classical Swahili Poem*. South Bend: Sahel Publishing Press.
- Olali, Tom. (2008b). *Performance of a Swahili Poem During the Lamu Maulidi Festival*. South Bend: Sahel Publishing Press.
- Olali, Tom. (2012). *Performing Arts in Lamu*. Berlin: Lambert.
- Olali, Tom. (2011). "The Place and Thematic Function of a Panegyric in Swahili Society: The Case of Sufi al-Busiri's *Kasida ya Hamziyya*." In Ogude J, Musila G and Ligaga D (eds) *Rethinking Eastern African Literary and Intellectual Landscapes*: New York: Africa World Press.